

Unadhania Unajua Msimamo wa Wakristo Uko Wapi Kuhusu Upangaji Uzazi? Fikiria Tena!



Akina mama na watoto wenye afya ndio nguzo la familia thabiti na, mwishowe, jamii dhabiti. Upangaji uzazi ni muhimu katika kuboresha afya ya akina mama na watoto kuititia upangaji unaofaa kati ya ujauzito na kuzuia ujauzito na uaviaji mimba usiohitajika.

Neno “Upangaji Uzazi,” kama linavyotumiwa na Christian Connections for International Health humaanisha kuwawezesha wapenzi kuamua idadi na muda wa ujauzito, ikiwa ni pamoja na matumizi ya kujitolea ya mbinu za kuzuia ujauzito, bila kujumuisha uaviaji mimba, ambazo ni sawa na maadili yao na imani ya kidini.

Je, kwa nini tuunge mkono Upangaji Uzazi?

Zaidi ya wanawake milioni 222 duniani wana hitaji lisilofikiwa la upangaji uzazi. Matumizi ya upangaji uzazi yanaweza kuboresha haraka afya na nafasi za kuisha kwa wanawake na watoto. Faida zinajumuisha:

- Kulinda afya ya watoto kwa kupunguza ujauzito wenye hatari ya juu.
- Kulinda afya ya watoto na akina mama kwa kuruhusu muda wa kutosha kati ya ujauzito.
- Kuwawezesha wanawake, ikiwa ni pamoja na wanawake wenye HIV, kulinda ujauzito usiohitajika.
- Kupunguza uaviaji mimba, ambao huchukua asilimia 13 ya maafa ya uzazi duniani.
- Kuwezesha familia kuwalinda vyema watoto wao.
- Wanachama wa CCIH wanajumuisha upangaji uzazi na shughuli zingine, kama vile kupima na huduma ya HIV/UKIMWI, kuzuia uambukizaji wa HIV kati ya mama na mtoto, na kama sehemu ya huduma za afya ya uzazi kwa wanawake wanaopokea huduma ya baada ya kujifungua na baada ya uaviaji mimba.

Hadithi kutoka Upande wa Kusini

Karibu km 5 nje ya Kampala, mji mkuu wa Uganda, kuna **Kliniki ya Hope Lukuli**. Iliyoanzishwa mwaka wa 2000, kliniki huu huudumia zaidi ya watu 60,000 katika umbali wa km 2. Huduma zake za upangaji uzazi hulenga kuwasaidia wanawake kuwa na ujauzito unaofaa na kaya kukua kwa kiwango wanachowea kumudu. Aina mbalimbali ya mbinu za upangaji uzazi zinapatikana kama vile ‘shanga za hedhi’ (Shanga, ambazo zinaunga mkono Mbinu ya Siku za Kawaida ili kutambua sahihi siku mwanamke yuko tayari kupata mimba katika mzunguko wa hedhi), mipira ya kondomu, tembe, sindano, na vibandikiza. Hizi zote hujadiliwa na kuchaguliwa na watu, kulingana na imani na mahitaji yao wenyewe. Wafanyakazi Waisilamu, Waangilikani, Wakatoliki hutoa ushauri na maelezo yanayounga mkono uaminifu katika ndoa. Mchanganyiko wa ufadhili kutoka Marekani, serikali zingine, na wafadhili wa kibiniasi wamesaidia kliniki kuhudumia jamii. Kwa habari zaidi, tembelea <http://www.ccih.org/Hope-Clinic-Uganda-Case-Study.pdf>.

Phyllis Joy Mukaire, Mkurugenzi Mkuu wa **Christian Health Association of Sudan** anaona upangaji uzazi kama sehemu muhimu ya kulinda afya ya wanawake na watoto na mustakabali wa uchumi ya taifa.

“Upangaji uzazi utazuia ujauzito usiopangiwa na kupunguza idadi ya uaviaji mimba, ambayo ni sababu kuu ya maafa ya uzazi na kutokuendelea nchini Sudani Kusini,” anasema. “Unaweza pia kusaidia kupata faida ambazo hufanyika wakati idadi ya watu wenye umri wa kufanya kazi inaongezeka ikilinganishwa na waliowachanga.”

Kiwango kinachopungua cha uzazi huboresha mgao wa wafanyakazi ikilinganishwa na kuwategemea watoto. Ijulikanao kama “mgao wa idadi ya watu”, picha hii husababisha ukuaji wa haraka wa uchumi na hupunguza baadhi ya ugumu ulio kwenye familia. Lakini kusaidia familia kupanga kuwazaa watoto wao ili ujauzito uweze kupewa muda unaofaa na familia kukua kwa kiwango ambacho wanawea kukimudu ni changamoto.

Kulingana na Mukaire, asilimia 3 tu ya wanawake nchini Sudani Kusini hutumia mbinu za kisasa za upangaji uzazi, na mwanamke wa Sudani Kusini ana wastani wa watoto 6.7 katika maisha yake.

Mukaire anaona ufikiaji mkubwa wa matoleo na maelezo ya upangaji uzazi kama jambo muhimu katika kushughulikia kiwango kikubwa cha uzaji katika Sudani Kusini na kiwango husika cha maafa ya uzaizi ya vifo 2,054 kwa watoto 100,000 wanaozaliwa wakiwa hai, kiwango cha juu zaidi duniani.

Christian Relief and Development, Inc. (CRDI) ni mfano mwagine wa shirika la Kikristo linalofanya kazi kufikia mahitaji ya wanawake ya kupanga uzazi wao. CRDI huendesha kliniki ambayo hutoa upangaji uzazi katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) ambayo ina kiwango cha maafa ya uzazi cha vifo 540 kwa watoto 100,000 wanaozaliwa wakiwa hai na kiwango cha uzazi cha watoto 5.8 kwa kila mwanamke.



Kulingana na Armand Utshudi, mwanzilishi na rais wa CRDI, bila ufikiaji huduma za upangaji uzazi, ujauzito usiotarajiwa na wa karibu sana ni tishio kwa wanawake katika maeneo ya mashambani ya DRC. "Watoto wa akina mama wanaojifungua kabla ya mtoto wao wa mwisho kufikia miaka miwili wanaweza kusumbuka na utapiamlo kwa sababu mtoto hapokei maziwa ya mama kwa muda unaofaa na lishe inayofaa ya ziada," anafafanua. "Wakati utapiamlo unapowaathiri watoto na akina mama, kinga zao mwilini hudhoofika na kuwa zinazoweza kuathiriwa na maambukizo ya kawaida, ambayo mara kwa mara husababisha magonjwa na vifo."

Uchunguzi umeonyesha kwamba watoto katika nchi zinazokua wana hatari ya juu zaidi ya kufa kama mama yao atafariki, au ana ndugu walio karibu sana kiumri. (*Picha hapo juu: (Mfanyakazi wa kliniki akimpima mwanamke mjamzito katika kliniki ya CRDI.)*)

Maombi

1. Kuunga mkono ufadhilli wa upangaji uzazi wa kimataifa kwa mashirika ya umma, kibinagsi, na ya imani ili kusaidia kupunguza hitaji lisilofikiwa la wanawake wanaotafuta upangaji uzazi, lakini hawana. Kufadhili huduma za upangaji uzazi za kimataifa hupunguza ujauzito na uaviaji mimba usiokusudiwa katika nchi masikini sana zenye hitaji kuu zaidi.
2. Kutambua umuhimu wa mashirika ya imani katika kutoa huduma za afya za kimataifa. Kuunga mkono ufadhilli wa mashirika ya imani katika kiwango kinacholingana na uchangiaji wao wa jumla wa huduma za afya ili kukuza huduma kamili ya afya, ikiwa ni pamoja na upangaji uzazi.

Kwa maelezo zaidi kuhusu CCIH na kazi ya Wakristo katika upangaji uzazi, angalia <http://tinyurl.com/CCIHResources>

CCIH | www.ccih.org | Christian Connections for International Health ni shirika la 501(c)3 la wanachama ambalo mtandao wake wa duniani unajumuisha zaidi ya watu 350 na mashirika 200 (Wakristo na mashirika husiani). Mtandao wa CCIH unajumuisha jamii pana ya watu waliojitelea kwa ndoto ya ulimwengu ambapo kila mtu anaweza kufikia huduma za afya ya kawaida na uzuiaji. | Kwa masali au maelezo zaidi, wasiliana na ccih@ccih.org



Ilisashisha Mwisho Oktoba 2013

Chapisho hili limewezeshwa na msaada kutoka kwa Wakfu wa Umoja wa Mataifa. Machapisho na maoni yote yatakayofuata yako chini ya uwajibikaji wa Christian Connections for International Health.